

RIPOTI YA KAMATI YA MAENDELEO YA WANAWAKE, HABARI NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR YA MWAKA 2017/2018

SEHEMU YA KWANZA:

0:0 UTANGULIZI

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Habari na Utalii, ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 106 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016.

Majukumu yanayotakiwa kutekelezwa na Wajumbe wa Kamati katika kipindi chote cha uhai wa Kamati hii, ni kama yalivyoelezwa katika Jadwali la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016. Majukumu hayo ni haya yafuatayo:

Kamati za Kisekta zitakuwa na majukumu yafuatayo:-

- (i) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliyotangulia.
- (ii) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.
- (iii) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na miradi ya wananchi ya Wizara husika.
- (iv) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.
- (v) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.
- (vi) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.
- (vii) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia katika utekelezaji wa ahadi hizo.
- (viii) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake , Habari na Utalii ambapo katika ripoti hii inajulikana kama "Kamati" inawajibu wa kufuatilia utekelezaji wa wizara mbili za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar , ikiwa ni pamoja na Idara, Mashirika, Kamisheni, Tume na Vitengo vilivyo chini ya Wizara hizo. Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii ni kama zifuatazo:-

- 1) Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo; na
- 2) Wizara ya Kazi, Uwezesaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

0:1 MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Kamati ilifanya kazi zake katika mizunguko mitatu kama ifuatavyo;-

1. Kuanzia Agosti 14 hadi Agosti 25 , 2017 - Unguja,
2. Kuanzia tarehe 14 Novemba hadi tarehe 24 Novemba, 2017 Pemba.
3. Tarehe 15/01/2018 hadi tarehe 26/01/2018 Unguja.

Aidha Kamati kwa kushirikina na Wizara husika ilipata fursa ya kutembelea Mikoa ya Dar es Salaam na Tanga kwa nyakati tofauti ili kujifunza kwa vitendo na hatimae kuweza kuishauri serikali ipasavyo kuhusiana na Sekta za Utalii, Utamaduni na Mambo ya Kale, Usalama na Afya Kazini, Maendeleo ya Wanawake na Watoto pamoja, Ushirika na Ajira.

0:2 WAJUMBE WA KAMATI

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake , Habari na Utalii inaundwa na Wajumbe wafuatao;-

- | | |
|------------------------------------------|-------------------|
| 1. Mheshimiwa Ali Suleiman Ali (SHIHATA) | Mwenyekiti |
| 2. Mheshimiwa Salha Mohammed Mwinjuma | Makamu Mwenyekiti |
| 3. Mheshimiwa Hassan Khamis Hafidh | Mjumbe |
| 4. Mheshimiwa Maryam Thani Juma | Mjumbe |
| 5. Mheshimiwa Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 6. Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub | Mjumbe |
| 7. Mheshimiwa Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| 8. Ndugu Himid Haji Choko | Katibu |
| 9. Ndugu Mussa Issa Mussa | Katibu |
| 10. Ndugu Amina Abeid Hemedi | Mkalimani |

0:3 HADIDU REJEA

Katika Utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2017/2018 kamati ilitumia hadidu rejea zifuatazo;-

- a) Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984.
- b) Kanuni za Baraza La Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2012.
- c) Hansard za Baraza za Mwaka 2016/2017,
- d) Ripoti za Kamati ya Mwaka 2016/2017
- e) Hotuba za Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii.

SEHEMU YA PILI

(1) WIZARA YA HABARI, UTALII, UTAMADUNI NA MICHEZO

1:0 Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo

Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ina jukumu la kusimamia sekta kuu nne katika nchi yetu. Sekta hizo ni za Habari, Utalii, Utamaduni na sekta ya Michezo.

Kamati inafahamu kwamba Malengo Makuu ya Wizara hii ni kuwa na maendeleo ya Habari, Utalii na Utamaduni na Michezo nchini kwa kuhakikisha mambo yafuatayo;-

- (a) Wananchi wanapata taarifa za kutosha na za usahihi kwa wakati muwafaka.
- (b) Wananchi wanashiriki katika kutangaza Utamaduni wa Zanzibar
- (c) Wananchi wanashiriki katika kazi za sanaa.
- (d) Kuhakikisha kwamba Zanzibar ni miongoni mwa nchi bora katika ukanda wa Bahari ya Hindi kwa masuala ya Utalii.
- (e) Kuhakikisha kwamba wananchi wanashiriki katika michezo kwa kushinda na kujenga afya.

Wizara inatekeleza majukumu hayo kupitia taasisi 15 kama zinavyoonekana hapa chini;-

- (1) Idara ya Uendeshaji na Utumishi
- (2) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
- (3) Idara ya Habari Maelezo
- (4) Idara ya Makumbusho ya Mambo ya Kale
- (5) Kamisheni ya Utamaduni na Michezo
- (6) Ofisi Kuu Pemba
- (7) Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC)
- (8) Shirika la Magazeti ya Serikali
- (9) Chuo cha Uandishi wa Habari
- (10) Tume ya Utangazaji
- (11) Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX)
- (12) Baraza la Kiswahili
- (13) Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU)
- (14) Baraza la Taifa la Michezo (BMTZ) na
- (15) Kamisheni ya Utalii.

1:1 BAJETI YA WIZARA:

Kwa mwaka wa fedha **2017/2018**, Wizara imetengewa jumla ya shilingi **19,385,656,000** na kwa upande wa makusanyo ilikadiriwa kukusanya shilingi **6,178,303,000** ambapo kati hizo **Tsh.4,468,303,000** ni mapato yanayoingia katika mfuko mkuu wa serikali (Hazina) na **Tsh.1,710,000,000** ni mapato yanayotumiwa na taasisi husika.

Utekelezaji halisi hadi kufikia Disemba 2017(Nusu Mwaka) ni kuwa makisio ya mapato kwa taasisi zinazotumia mapato ni **Tsh.890,240,000** na zilikusanywa **Tsh 959,348,287** sawa na asilimia 107. Kwa upande wa mapato yanayoingizwa hazina makisio kwa Kipindi cha Julai-Disemba ni **Tsh.567,848,000** na zilizokusanywa ni **Tsh.401,743,110** sawa na asilimia 71.

1:2 SEKTA YA HABARI

Sekta ya Habari ni moja kati ya sekta muhimu sana katika jamii yoyote duniani kwani hutumika kuuhabarisha Umma, kuhusu mambo mbalimbali yanayoendelea yakiwemo ya kisiasa, kiafya, kielimu na hata kiuchumi. Aidha Sekta hii hutumika kuibua, kueleza, kufafanua na hata kuburudisha katika jamii.

Habari ina nafasi kubwa kwani inawezesha watu katika jamii husika kupata taarifa, habari na maarifa na hatimae kuzitumia kwa kudadisi na kuhoji, kufikiri zaidi na kupembua na hatimae kuwa na maoni yatakayomuwezesha kufanya maamuzi sahihi juu ya kile ambacho kinawagusa au kuwahusu.

Taifa lenye watu wenye kupata habari sahihi na kwa wakati sahihi linakua vizuri katika nyanja mbalimbali kama vile kiuchumi, kisiasa kijamii na hata kiutamaduni.

Sekta hii kwa ujumla wake bado inakabiliwa na changamoto kadhaa zinazohitaji kufanyiwa kazi, ili hatimae iweze kutekeleza majukumu yake ya msingi katika kuhabarisha, kuelimisha na kuiburudisha jamii. Licha ya juhudi kubwa zinazochukuliwa na watumishi waliomo kwenye sekta ya Habari, Kamati imebaini kwamba bado utendaji wao wa kazi umekuwa unakumbwa na vikwazo kadhaa kufanikisha majukumu yao kwa ufanisi ikiwemo mazingira magumu ya kufanyia kazi, Uhaba wa vitendea kazi vya kisasa,wataalamu, mafunzo katika maeneo yao ya kazi na maslahi yasiyoendana na ukubwa wa majukumu yao kwa jamii na taifa kwa ujumla.

1:2 : 1 SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC)

Shirika la Utangazaji Zanzibar yaani *Zanzibar Broadcasting Coperation (ZBC)* ni muungano wa zilizokuwa taasisi *mbili (2)* kubwa za habari nchini ambazo ni: Sauti ya Tanzania Zanzibar (*STZ*) na Idara ya Televisheni (*TVZ*). Taasisi hizi ziliunganishwa kupitia Sheria ya Shirika la Utangazaji Zanzibar, nambari 4 ya Mwaka 2013.

Majukumu makuu ya Shirika hili ni: kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha. Mbali ya majukumu hayo, kamati imebaini kwamba pia, Shirika ni mdomo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa lengo la kuiweka karibu na wananchi kwa mustakabali wa nchi hii.

Kwa mantiki hiyo Kamati inaitaka ZBC ijitambue kwamba ni vyombo vya utangazaji vya Taifa ambapo bado wananchi wengi wanapenda kuangalia na kuisikiliza. Hivyo basi pamoja na ushindani wa vyombo vya habari uliokuwepo, ZBC inapaswa kuendeleza **“Tone”** yaani lafudhi yake ambayo imekua ikiendeleza hadhi yake kwa muda mrefu sasa pamoja na matumizi ya lugha kwa ufasaha. Niukweli usiopingika kwamba kuna baadhi ya watangazaji bado usomaji na utangazaji wao hauridhishi kwa kudodosa dodosa baadhi ya maneno. Pia Kamati imebaini kuweco kwa malamiko kadhaa yanayohusiana na nyimbo, vipindi na baadhi ya maudhui yanayooneshwa au kusikilikana kwamba, hayana au hayafunzi maadili mazuri kwa utamaduni wa Mzanzibari na Tanzania kwa ujumla.

Kamati inatoa mfano wa kipindi cha ‘Burdani’ Cha ZBC Redio saa 8:00 Mchana kiendeleo kuwa cha Burdani badala ya kuweka Mipasho Mikali na malumbano, Kipindi Cha ‘Ugua pole” watangazaji wake waonekane kuwa na Upole na Unyenyekevu kwa wagonjwa na Taarifa za habari zisomwe na wasomaji ambao tunahisi kweli wanaweza kusoma taarifa hizo kwa ufasaha na si kwa kuwalazimisha.

Kamati ilitembelea Studio za ZBC – Karume House, Rahaleo, Mkorosheni Pemba na Dare es Salaam pamoja na Mitambo ya kurushia matangazo ya Masingini ,Dole na Bungi ambapo kwa ujumla Kamati imebaini kwamba hali ya rasilimali watu na Vitendea Kazi katika vituo vyote hivyo sio nzuri, huku ikiwa na mlolongo wa wafanyakazi wa kujitolea ambapo hadi kufikia Mwezi Disemba 2017, ZBC inawafanyakazi ambao hawajaajiriwa wamefikia 53.

Mafanikio ya ZBC

- (a) Shirika limepatia mitambo mipya ya kisasa pamoja na ukarabati mkubwa wa studio za Redio na Karume House
- (b) Katika kipindi cha kuanzia *Julai hadi Disemba 2017*, ZBC imeweza kuongeza wigo wa kutayarisha vipindi vingi vya ndani ambavyo vinagusa maisha ya jamii kama vile vuna kipaji, kutoka majimboni, safari nk.
- (c) Shirika limeweza kununua (*Server*) kwa ajili ya kuhifadhi hotuba za viongozi wa kitaifa, nyimbo za zamani katika mfumo wa kisasa na uhifadhi ulio bora zaidi.

Mambo ambayo Kamati haikuridhika nayo na Changamoto kuhusiana na ZBC

- **Usafi** : Kamati haikuridhika kabisa na hali ya usafi na utunzaji wa vifaa vipya na vya kisasa kabisa katika Studio za Mkorosheni Pemba pamoja na Karume House ambapo, inawasiwasi kwamba huenda vifaa vya studio hizo ambayo vimeigharimu taifa fedha nyingi sana visifike muda wake wa matumizi uliokadiriwa kutokana na utunzaji mbovu wa vifaa hivyo.
- **Kutapakaa wa Waya Studio** : Mpangilio usiorasmi na kutapakaa kwa waya kila pahala hasa katika Studio za kurikodia watu Maalum (VIP) ni miongoni mwa mambo ambayo hayatoi taswira nzuri Kituoni Shirikani hapo.
- **Ujenzi wa jengo Jipya Pemba** :Taarifa za Ujenzi wa jengo jipya Pembezeni mwa Studio ya zamani ya Mkoroshoni Pemba ambalo litakua Karibu mno wa jengo la zamani pia litakaribiana sana na barabara.
- **Madeni**: Kutolipwa kwa malimbikizo ya mfanyakazi **Khamis Dadi Khamis** wa ZBC Pemba kwa muda mrefu sasa huku kukiwa na taarifa zinazokinzana kuhusiana na malipo hayo kutoka kwa viongozi wa Wizara na Viongozi wa Shirika.
- **Ajira** : Mwenendo wa ajira hasa ZBC TV ambapo huaajiri wafanyakazi wapya na kuwaacha vijana wanaowatuma kwa kujitolea kwa kipindi kirefu.

- **Malipo ya Wafanyakazi wanaohudhuria Mikutano ya BLW.** : ZBC Kutowalipa ipasavyo na kwa wakati kwa wafanyakazi wanaohudhuria katika Mikutano ya Baraza la Wawakilishi.

MAAGIZO YA KAMATI

- 1)** ZBC ihakikishe kwamba inasawazisha deni la malimbikizo ya mafao ya Wafanyakazi wake Unguja na Pemba
- 2)** ZBC iandae mpango maalum wa Usafi na utunzaji wa Vifaa vipya hasa katika Studio za Mkanjuni na Karume House.
- 3)** ZBC iwe na mpango maalum wa kuwapa mafunzo watangazaji wake, ili kupunguza tabia ya kukosea kosea kwa baadhi ya Watangazaji wake.
- 4)** ZBC iwalipe ipasavyo na kwa wakati kwa wafanyakazi wanaohudhuria katika Mikutano ya Baraza la Wawakilishi.

1:2: 3 SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI

Shirika la Magazeti ya Serikali ni wachapaji wa magazeti ya kila siku ya Zanzibar Leo, Zanzibar Leo Jumapili na ZanSport. Shirika limeanzishwa mwaka 1998 ambako kulifuta gazeti la Nuru lililokuwa likitolewa kila wiki. Gazeti la Nuru lilianzishwa mwaka 1992.

Mafanikio Shirika la Magazeti ya Serikali

Kamati imebaini kwamba Tokea kuanzishwa kwake, Shirika limeweza kupata mafanikio mengi ikiwa miongoni mwao ni kama yafuatayo:-

- (a)* Gazeti la Zanzibar Leo saa linachapwa Zanzibar na Wakala wa Uchapaji (ZAGPA) kuanzia tarehe 10 Mei, 2017.

- (b) Shirika limefanikiwa kubadili muonekano wa gazeti na kuwa na mvuto zaidi pamoja na kuongeza kurasa kutoka kurasa 16 hadi 24.
- (c) Gazeti la Zanzibar Leo limekuwa likiandika habari nyingi za Zanzibar kulinganisha na magazeti yote ya Tanzania.

Mambo ambayo Kamati haikuridhika nayo na Changamoto za Shirika la Magazeti ya Serikali

Kamati imegundua kwamba licha ya mafanikio ya hapo juu Shirika katika utekelezaji wa majukumu yake linakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- (a) **Tatizo la usafiri:** Shirika linakabiliwa na tatizo kubwa la usafiri katika kufanikisha shughuli zake za kila siku. Shirika lina gari *nne (4)* na vespa ilizorithi kutoka gazeti la Nuru tokea mwaka 1992.
- (b) **Madeni :** Hadi sasa Shirika linadai *Tshs. 323.2 milioni* katika taasisi mbalimbali. Taasisi za Serikali zinadaiwa *Tshs. 184.5 milioni* na zile za binafsi zinadaiwa *Tshs. 138.7 milioni*.
- (c) **Mtaji ;** Kamati inaona ingelikuwa vyema na busara zaidi kwa Shirika kama hili lingeanza na mtaji ambao ungesaidia kusimamia shughuli za maendeleo na mapato kuliko kusubiri ruzuku na mauzo ya magazeti.
- (d) **Kutokuwa na uhakika wa idadi za nakala za uchapaji:** Kamati ya Maendelo ya Wanawake, Habari na Utalii imebaini kwamba Wakala wa Uchapaji ambaye ndiye mchapaji wa gazeti la Zanzibar Leo ameshindwa kuwa na idadi kamili ya uchapaji wa nakala ambazo zimekubaliwa na Serikali pamoja na Shirika.

Kamati iliarifiwa kwamba Nakala zilizokubaliwa ni 3000 kwa siku. Hata hivyo, kuanzia *Agosti 11, 2017*, nakala za Zanzibar Leo zimekuwa zikipungua kwa sababu tofauti kama mfano;-

Nam.	Tarehe	Idadi ya Nakala
1.	<i>11 Agosti, 2017</i>	<i>1500</i>
2.	<i>12 Agosti, 2017</i>	<i>940</i>
3.	<i>13 Agosti, 2017</i>	<i>420</i>
4.	<i>15 Agosti, 2017</i>	<i>520</i>
5.	<i>16 – 23 Agosti, 2017</i>	<i>1000</i>

(e) Gazeti kuchelewa kupelekwa Tanzania Bara na athari zake

Shirika lilianza rasmi kuchapisha gazeti lianze kwa Wakala wa Uchapaji Zanzibar kuanzia tarehe 10 Mei, 2017. Hata hivyo, Kamati iliarifiwa na Shirika kwamba Shirika kumekua na athari pamoja na changamoto nyingi zilizotokezea baada ya kuanza kutekeleza maamuzi hayo. Katika changamoto na athari hizo kubwa ni:

(i) Kushindwa kufika gazeti Dar es Salaam na mikoani kwa wakati

- Gazeti linashindwa kupelekwa Dar es Salaam kwa wakati kutokana na mchapaji kushindwa kuliwasilisha gazeti kabla ya muda unaowiana na vyombo vya usafiri wa kwenda Dar es Salaam.
- Shirika linalazimika kutumia usafiri wa Azam marine kwa boti yake ya mwanzo ambayo huondoka siku ya *pili (2)* saa *01:00* asubuhi na kufika Dar es Salaam saa *03:00* asubuhi.
- Vyombo vya habari vinavyosoma muhtasari wa magazeti kwa njia ya redio na televisheni haviwahi kupata gazeti hili kwa wakati jambo linalopelekea gazeti la leo kusomwa kesho yake.

(ii) Kufa kwa soko la Tanzania Bara

- Gazeti linakuwa 'kiporo' na wateja wanakuwa wazito kununua gazeti ambalo habari zake zimeshapitwa na wakati kwa kuwa wanakuwa wameshapata kupitia vyombo vyengine.
- Licha ya soko kufa lakini kuna hasara kubwa ya malipo ya kusafirisha gazeti ambapo tija yake inakuwa ndogo kuliko hasara.

(iii) Kukosekana kwa matangazo ya biashara kutoka Tanzania

Bara: Gazeti linaingiza mapato mengi kutokana na matangazo ambapo matangazo mengi yanayotangazwa katika gazeti letu ni kutoka Tanzania Bara. Gazeti litakuwa si la kuaminika katika matangazo ya wateja (kwa mfano hotuba za bajeti katika Bunge la Tanzania ambapo machapisho yalikuwa yakiingiza wastani wa *Tshs. 10 milioni* kwa kila hotuba).

(f) Propaganda haitakuwa kwa ufanisi: Kiini cha propaganda ni tukio na wakati. Kukosekana kimoja wapo kati ya hivyo, dhana hiyo haiwezi kutekelezeka. Kwa hivyo, lengo la gazeti hili la kuwa chombo kikuu cha propaganda kwa sera za Serikali linazorota.

MAAGIZO YA KAMATI

(a) Shirika la Magazeti ya Serikali liimarisha kitengo chake cha Biashara, Masoko na Matangazo ili kuhakikisha kuwa soko la Zanzibar Leo linaimarika Tanzania nzima.

(b) Shirika lirudishe tena gazeti la ZanSport lililokuwa likiandika zaidi habari za burudani na utalii.

(c) Shirika lihakikishe kwamba gazeti lake la Zanziabar linatoa habari za Michezo hasa mwenendo wa Ligi Kuu ya Zanzibar mpira wa Miguu ikiwa ni njia moja wapo ya kurudisha ari na ushahihishaji wa mchezo huo hapa nchini.

1:2: 4 Idara ya Habari Maelezo

Idara ya Habari Maelezo ni miongoni mwa taasisi zilizomo katika Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Zanzibar ambayo imeundwa rasmi tarehe *16 Machi 1996* kutoka iliyokuwa Idara ya Habari na Utangazaji. Miongoni mwa majukumu ya idara hii ni kama yafuatayo:-

- (i) Msemaji Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.
- (ii) Kusimamia kutoa vitambulisho kwa waandishi wa habari na wapiga picha wa ndani na nje ya nchi wanaofanya shughuli zao Zanzibar.
- (iii) Kuwaelekeza waandishi wa habari watakaofanyakazi Zanzibar, maadili, maeneo na mipaka yao ya utendaji wa kazi.

Mambo ambayo Kamati haikuridhika nayo na Changamoto za Idara ya Habari Maelezo

Kamati ilitembelea makao Makuu ya Idara ya Habari Maelezo Rahaleo ambapo pamoja na utekelezaji wake wa makujumu ya kila siku, kamati haikuridhishwa na mambo yafuatayo;-

- Kukosekana kwa mfumo bora wa utunzaji wa kumbukumbu za Picha na vielelezo vyengine muhimu kuhusiana na viongozi wetu wa Kitaifa.
- Utendaji wa Idara hii kusuasua na hatimae kuonekana kwamba majukumu ya Idara hii yanafanywa na watu ama taasisi nyengine.
- Baadhi ya Taasisi Kutoitumia ipasavyo Idara hii hasa wanapokuwa wanahitaji kusambaziwa habari zao au mikutano ya waandishi wa Habari (Press Conference) ama wanapokuwa matukio na kazi zinaotakakiwa kutangazwa kwa jamii.
- Baadhi ya Kauli na matamshi ambayo hayana maadili ama heshima dhidi ya viongozi kwa Baadhi ya Maafisa wa Idara hiyo.
- Kutokuwa na ushirikiano na mfumo bora wa mashirikiano na Vyombo vya habari vya watu binafsi.

MAAGIZO YA KAMATI.

- (i) Idara ifikirie kuweka na kufanyakazi mabango ya kielektroniki na katika Maeneo yenye mkusanyika mkubwa wa watu ili kusambaza zaidi taarifa mbali mbali zinazohusu serikali na jamii kwa Ujumla.
- (ii) Idara iweke Ubao wa Picha na matangazo (Display Board) katika Katika Ofisi za Baraza la Wawakilishi Chukwani kama ilivyokuwa hapo kabla huko Kikwajuni.
- (iii) Idara izidi kujitangaza kwa taasisi mbali mbali za serikali na Binafsi ili majukumu ya Idara hiyo yazidi kufahamika.
- (iv) Idara ihakikishe kwamba Wanahabari wote wanakata leseni zao (Press card) kila mwaka ili kuondosha usumbufu na malumbano yanayotokea baadhi ya wakati wanapokwa wanatekeleza majukumu yao.

1:2:5 Tume ya Utangazaji Zanzibar

Tume ya Utangazaji ni taasisi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliyoanzishwa mwaka 2002 kwa Sheria nambari 7 ya mwaka 1997. Kwa mujibu wa Sheria, Tume imepewa majukumu ya kuruhusu, kusimamia na kukuza vyombo vya utangazaji vyenye kuwa na uhariri wake wenyewe wa ndani na bila ya kuingiliwa katika masuala ya msingi ya uendeshaji wa shughuli zake.

a) Hali ya watendaji katika Utangazaji

sekta ya utangazaji imesaidia kutoa ajira kama ilivyotarajiwa katika malengo ya Sera na Sheria ya Utangazaji Zanzibar. Hadi kufikia *Disemba* , 2017, sekta hii imekuwa na watendaji 714 kwa upande wa redio na televisheni binafsi na wafanyakazi 346 kwa upande wa redio na televisheni ya umma.

b) Utekelezaji wa majukumu ya Tume

Kamati inapongeza utekelezaji wa Tume katika Kipindi hiki, ambapo imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

- (a) Tume imekamilisha utayarishaji wa Kanuni za Utangazaji ambazo zinaweka utaratibu wa utoaji wa leseni za huduma ya utangazaji na biashara ya utangazaji.
- (b) Tume sasa inaandaa Kanuni za Maudhui ya Mitandao ya Kijamii kutokana na kuwepo kwa wawekezaji wanaotaka kujisajili na kutoa huduma za redio na televisheni katika mitandao. Hatua hii itasaidia katika kubadili changamoto ya sekta ya habari kwa njia ya mitandao ya kijamii ambayo imeshamiri nchini.
- (c) Tume imeandaa rasimu ya mwongozo wa viwango vya ukomo wa ada ya usambazaji wa maudhui.

Mambo ambayo Kamati haikuridhika nayo na Changamoto katika Tume ya Utangazaji

- Ukosefu wa miundombinu ya kufuatilia na kuweka kumbukumbu za maudhui yanayorushwa na vituo mbalimbali.
- Ukosefu wa mawimbi ya kutangazia kwa upande wa redio kwa wawekezaji wapya. Idadi ya vituo vya redio viliopo imemaliza kabisa mgao wa mawimbi ya kutangazia ya *FM* na hivyo kuwakosesha wawekezaji wapya kuanzisha vituo vya redio.
- Televisheni ya Taifa ya Zanzibar (ZBC TV) kufungwa katika baadhi ya ving'amuzi mara tu baada ya kumalizika kwa muda wa malipo.

c) Vyombo vya Habari vya Binafsi

Kamati ilipata Fursa ya kukutana na Wamiliki wa Vyombo vyote vya habari Hapa Zanzibar pamoja na kutembelea Baadhi ya Vituo Binafsi vya Matangazo ya Redio na TV ikiwemo Zanzibar Cable, Bahari FM, Redio Al-nour FM na Redio Istiqama FM pamoja na Pemba Cable TV ambapo ilipata fursa ya kuangalia shughuli za Utendaji wa Taasisi hizo ambapo kwa kiasi Kamati imeridhishwa na Utendaji wa Vyombo hivyo.

Kwa ujumla Kamati imegundua kwamba katika vyombo vya habari vya watu binafsi kumekua na ufanisi wa kazi na vimejipanga vizuri. Hivyo, Kamati inawasiwasi kwamba kutokana na mwenendo uliopo hivi sasa, vyombo vya serikali vinaweza kukimbiwa na wasikilizaji na watazamaji.

Changamoto za vyombo vya Habari Vya Binafsi;

- (a) Vyombo vya habari vinakabiliwa na gharama kubwa za umeme pamoja na umeme huo ama kukatika mara kwa mara au kuwa mdogo hali inayohatarisha kuungua na kuharibika kwa mitambo yao mara kwa mara.
- (b) Vilevile, ilielezwa kuwa, mara kadhaa vyombo vya habari vya binafsi havishirikishwi katika shughuli nyingi za Serikali zikiwemo ziara za viongozi wakuu wa Serikali, mikutano na kadhalika.
- (c) Vyombo vya habari vya binafsi vimelalamikia gharama kubwa za kukodi minara ya kurushia matangazo yao katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba ambapo kwa sasa vinakodi kwa *Tshs. 7,000,000* pamoja na leseni za biashara zao.

d) Vituo vya Redio Jamii.

Kamati imefurahishwa na mwamko wa jamii mbali mbali wa kuanzisha vituo vya Redio jamii hapa Zanzibar , kwani Kamati inaamini kwamba ni muhimu na vinasaidia kushajihisha jamii husika katika masuala mbalimbali ya kimaendeleo, burdani na michezo na ustawi wa jamii zao.

Kamati ilitembelea baadhi ya vituo hivyo ikiwemo Micheweni FM, Mkoani FM ambapo iliarifiwa kwamba kumekua na uelewa mdogo wa wanavijiji katika kuchangia gharama za uendeshaji wa vituo vya redio jamii katika maeneo yao, hivyo kuhatarisha uendeshaji wa Redio hizo.

e) Vyama /Vilabu vya Waandishi wa Habari.

Katika kuhakikisha kua tathnia ya Habari hapa Zanzibar inaimarika, waandishi wa Habari wameamua kujikusanya kwa pamoja na kuunganisha nguvu zao kwa kuunda vyama na vilabu mbali mbali. Wakati wa kazi za Kamati , Kamati yetu ilitembelea na kukutana na vyama hivyo ikiwemo Pemba Press Club, Baraza la Habari Tanzania (MCT) Ofisi ya Zanzibar , Jumuiya ya Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Ofisi ya Zanzibar, Chama cha Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC), Jumuiya ya Waandishi Wachanga (UDEJO), WAHAMAZA na ZAMEO.

Kamati imegundua kwamba vilabu na Vyama hivyo zimeanzishwa kwa lengo la kukuza viwango vya taaluma ya uandishi wa Habari kwa wanachama wake na kuraghibisha mashirikiano miongoni mwa waandishi wa habari, vyanzo vya habari na jumuiya za kitaaluma.

Aidha Vilabu hivyo viko mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba Uhuru na haki ya kupata habari unalindwa, waandishi wa habari wanatekeleza vyema Wajibu wao (maadili) pamoja na Kufuatilia utendaji wa Vyombo vya habari.

MAAGIZO YA KAMATI.

- (a) Kamati inaitaka Tume kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na Serikali kwa ujumla ili kuidhinisha matumizi ya mawimbi yaliopo kwa ajili ya kuweza kukabiliana na upungufu wa mawimbi uliopo.
- (b) Kamati inaiagiza Tume ya Utangazaji na Wizara kwa ujumla kuangalia uwezekano wa kupunguza baadhi ya Kodi ikiwemo za minara, vifaa vya utangazaji na umeme wawekezaji wa sekta hii waweze kumudu vyema malengo yao.
- (c) Tume iwasiline na taasisi husika iii kuhakikisha kwamba waandishi wa Habari kutoka vyombo binafsi na wao wanashirikishwa katika ziara za kikazi za viongozi wakuu wa kitaifa japo kwa zamu pale hali inaporuhusu.
- (d) Tume kwa kushirikiana na wadau wa habari ichukue mikakati maalum ya kuhakikishwa kwamba watendaji katika kada ya Habari na Utangazaji wanatekeleza wajibu wao kwa kufuata maadili ya kazi zao, mila, silka na utamaduni wa nchi yetu.

1:3 SEKTA YA UTALII

1:3: 1 Kamisheni ya Utalii

Kamisheni ya Utalii imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Utalii, nambari 6 ya mwaka 2009 ambayo ilifanyiwa marekebisho na Sheria nambari 7 ya mwaka 2012. Majukumu ya msingi ya Kamisheni ya Utalii ni uratibu, usimamizi, utangazaji na uendelezaji wa sekta ya utalii hapa Zanzibar. Hadi kufikia Disemba 2017 Kamisheni imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 302,251,918 ambazo ni sawa na asilimia 94 ya Makadirio (321,588,000).

a) Mafanikio katika Sekta ya Utali

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, sekta ya utalii imepata mafanikio makubwa kama ifuatavyo:-

- (i) Kuongezeka kwa idadi ya wageni wanaoingia nchini kutoka wageni 376,342 (2016) hadi 433,166 sawa na ongezeko la asilimia 16%.
- (ii) Ujio wa ndege mpya na meli za kitalii.
- (iii) Kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaorudia matembezi yao.
- (iv) Kuandaa matamasha ya kitalii

Kwa nyakati tofauti kamati ilitembelea hoteli kadhaa za kitalii ikiwemi, Mtoni Marines, Kilindi Zanzibar, The Aiyana Hoteli- Makangale, Manta Resort – Makangale, Fundu Lagon – Mkoani, Ngalawa Hotel & Resort'- Kihinani, Zanzibar Serena Hotel, Mkonge Hotel - Tanga, Tulia Zanzibar Unique Beach – Pongwe, Whitesand Luxury Villa – Paje na Ndade Beach Lodge- Paje.

Mambo ambayo Kamati haikuridhika nayo na Changamoto za Utekelezaji Majukumu ya Kamisheni ya Utalii

- **Miundombinu** : Kamati imegundua kwamba takriban hoteli zote zinakabiliwa na tatizo la miundombini ikiwemo tatizo kubwa la barabara , maji safi na umeme usiokua wa uhakika.
- **Vitambulisho**: Kuchelewa kupatiwa vitambulisho kwa waongozaji na watembezaji watalii ambao huvilipia mapema kila mwaka.
- **Takwimu**: kukosekana kwa takwimu sahihi za Wageni wanaoingia nchini kwa shughuli za Kitalii suala ambalo linachangia upotevu wa mapato.
- **Warusha Vishada (KITE) Paje:**

b) Wadau wa Sekta ya Utalii.

Kamati pia ilikutana na Wadau wa Sekta hii wakiwemo Jumuiya ya Wawekezaji katika Sekta ya Utalii (ZATI) na Jumuiya ya Makampuni ya Watembezaji Watalii (ZATO), ZATOGA pamoja na jumuiya nyengine za sekta hii.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana na wadau hao wamelalamikia suala la *Maagent* wa nje kuwa na mashirikiano madogo na *Maagent* wa ndani, watembeza wageni ambao hawajasajiliwa (Mapapasi) pamoja na gari bubu zinazofanya shughuli za kitalii na baadhi ya sheria za Kazi, kwamba ni baadhi ya changamoto zinazozikumba jumuiya zao na kupunguza upatikanaji wa mapato yao na kupotea kwa wingi mapato ya serikali.

1:3: 2 Mgogoro wa wananchi wa Paje na Warusha Vishada vya Michezo ya Baharini (KITE)

Kamati ilifanya ziara maalum ya kuwatembelea wananchi wa kijiji cha Paje ambao wanalalamikia kutopata sehemu ya malipo kutokana na shughuli za urushaji wa Vishada vya baharini vinavyofanywa na wawekezaji na wanamichezo wa mchezo huo. Hali hii inatokana ya kuwa , wananchi wa Paje wameacha kufanya shughuli zao za kiuchumi walizokua wakizifanya baharini ikiwemo kusokota kamba (Vyau) , utafutaji wa Pweza (Bwachi) na Upandaji wa Mwani ili kupisha mchezo huo ikiwa ni njia moja wapo kuendeleza utalii . Hata hivyo, wamekuwa hawafaidiki na chochote kwa muda mrefu sasa huku warusha vishada wakiendelea kutononoka kutokana na mapato hayo ambapo hujipatia dola 20 kwa kurusha Kishanda Kimoja kwa saa moja , mapato ambayo hayana kodi yoyote inayoingia serikalini.

Kamati inawasiwasi kwamba hali hii ikiachiwa kuendelea inaweza kuzusha mgogoro mkubwa hapo baadae na kuleta athari mbaya kwa wanakijiji , wageni na serikali kwa ujumla.

1:3: 3 Utalii wa Ndani

Katika Kuijengea Uwezo Kamati, katika Masuala ya Utalii wa ndani Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Wizara iliandaa ziara ya kujifunza katika Bodi Ya Utalii Tanzania (Tanzania Tourism Board – {TIB}) Dar es Salaam, Hifadhi ya Taifa Saadani Tanga , Mapango ya Amboni - Tanga. Kamati imejifunza Mengi kutokana na ziara hizo ikiwemo;-

- Umuhimu mkubwa wa kuimarisha Utalii wa ndani kwani unanafasi nzuri ya kuongeza pato la Taifa.
- Umuhimu wa Kamisheni ya Utalii kuwasiliana na Wizara ya Elimu, ili kuangalia uwezekano wa kuwepo kwa Mtaala wa Utalii na hatimae kufundishwa katika Skuli za Msingi kama wanavyonfanya kwa baadhi ya Skuli huko Tanga.
- Kuanzisha ushirikiano wa Kamisheni ya Utalii ya Zanzibar na Hifadhi ya Saadani kwa kubadilishana Watalii kwa lengo la kuzitangaza Kiutalii pande zote mbili.
- Kuendeleza uhifadhi wa Uoto wa Asili pamoja na viumbe hai , katika hifadhi zetu ikiwemo Misitu na Magofu.

1:3: 4 Tatizo la Ukosefu wa Mafuta ya Petroli Disemba 2017

Pamoja na athari kubwa za kijamii, na hasara kubwa kwa wafanyabiashara, Makampuni na hata kwa Serikali , Sekta ya Utalii nayo ilipata pigo kubwa kutokana na ukosefu wa Nishati ya mafuta ya Petroli mwishoni mwa mwezi wa Disemba 2017, suala ambalo lilipelekea usafiri wa barabarani kuwa mgumu katika kipindi hicho. Baadhi ya watalii waliakhirisha safari zao za kuja Zanzibar na wengine waliokwisha kutangulia walibadilisha ratiba zao za ndani na kusababisha hasara kubwa ya mapato ambayo tulikua tunayategemea. Baadhi ya wageni walikosa ndege na kuakhirisha safari baada ya gari walizokua wakitegemea kuwachukua kutoka Hoteli hadi uwanja wa Ndege kukosa mafuta na kusababisha hasara kwa *Maagent wao*.

Kamati inawasiwasi kwa nini tatizo kama hili litokee katika mwezi wa Disemba, mwezi ambao sote tunafahamu kwamba wageni wengi huwa wanatembelea Zanzibar kwa mapumziko ya Krismass na mwaka mpya. Kamati inaishauri Serikali kuitafakari kwa kina Kadhia hii.

Aidha baadhi ya kauli zinazotolewa kwa wageni baadhi ya wakati sio nzuri na zenye kuwavunja moyo watalii wetu. Mfano mzuri ni wakati ule ule wa Kadh-ya

ya ukosefu wa Petrol, mtendaji mmoja wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Maji na Mafuta "ZURA" wakati akifanya uchunguzi wa mafuta katika sheli ya Kijangwani alimtolea maneno ya fedheha Mtalii kama alivyonukuliwa na mmoja wa Watembezaji wa Watalii wakati akitoa ushuhuda wake kwa Kamati kama ifuatavyo:- "***Next time do not do your holiday in Zanzibar...***" akimaanishwa kwamba wasije tena Zanzibar. Aidha uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba kauli na usumbufu kama huo mara nyengine huwa unajitokeza kwa watendaji wa Kamisheni ya Utalii, Jeshi la Polisi na watu wengine wanaoshughulika na wageni.

MAAGIZO YA KAMATI.

- (1) Kamisheni ihakikishe kwamba Sheria ya Utalii, nambari 7 ya mwaka 2012 inayoweka masharti ya kuweko kwa mfuko wa maendeleo ya vijiji, ambapo kila mwekezaji anapaswa kuchangia asilimia moja (1) ya mapato yake inatekelezwa.
- (2) Kamisheni ya Utalii kukaa pamoja na watendaji wa Idara ya Uvuvi, Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa ili kulipatia ufumbuzi endelevu Suala la urushaji wa Vishada Paje na kwengineko kwenye matatizo yanayofanana na hayo kwa lengo la kupata mfumo wenye tija kwa pande zote (wananchi, serikali na wawekezaji).
- (3) Kamisheni ya Utalii ipeleke maombi serikalini ili kuwepo Mtaala wa Masomo ya Utalii na kufundishwa tokea Skuli za Msingi.
- (4) Kamisheni ihakikishe inashirikiana na Halmashauri za Wilaya na Idara ya Mazingira ili kulitafutia ufumbuzi Suala la Uhifadhi wa taka taka za mahoteli badala ya mtindo wa hivi sasa wa kuzitupa mwituni na kuchafua mazingira.
- (5) Kamisheni ihakikishe kwamba wadau wote wanaotoa huduma za utalii wanalipa leseni za uendeshaji kwa wakati na kiwango sahihi.

1:4 SEKTA YA UTAMADUNI

Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo moja ya majukumu yake ya msingi ni kuhakikisha kuwa utamaduni wa nchi yetu unahifadhiwa na kulindwa kwa maslahi ya kizazi cha sasa na cha baadae. Katika kufanikisha hilo zipo taasisi mbali mbali kisheria ambazo zina wajibu wa kuyashughulikia mambo ya mila, silka na utamaduni wetu. Taasisi hizo ni kama zifuatazo:-

- i. Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni
- ii. Baraza la Kiswahili
- iii. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale.

Kamati ilivitembelea vyombo hivyo vyenye jukumu la kusimamia Sanaa, Lugha ya Kiswahili, Urithi wa Makumbusho na Mambo ya Kale pamoja na Utamaduni.

1:4:1 Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni

Kamati ilitembelea Ofisi za Baraza Mwanakwerekwe Zanzibar na kubadishana mawazo juu ya suala zima la Sanaa, jinsi ya uhakiki wa filamu unavyofanyika na njia wanazotumia kuhakikisha kuwa utamaduni wetu unahifadhiwa.

Mambo ambayo Kamati haikuridhika nayo;-

- ✓ **Matumizi sahihi ya Lugha ya Kiswahili:** Hivi sasa kumekua na matumizi ya maneno kadhaa ya Kiswahili ambayo sio sahihi huku katika sehemu mbalimbali ikiwemo Vyombo vya Habari huku Baraza la Kiswahili likifumbia macho makosa hayo.
- ✓ **Filamu zisizo na maadili :** Baadhi ya filamu zenye maudhui na taswira isiyokubalika katika maadili yetu kuoneshwa katika Vituo vyetu au kuzagaa katika maduka ya Kanda za Vedio .
- ✓ **Ufuatiliaji Mdogo:** Kumekua na ufuatiliaji mdogo katika maeneo yanayooneshwa kazi za sanaa ya Filamu na Utamaduni kutokana na kukosekana kwa usafiri wa uhakika ambapo kwa mujibu wa kazi za Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni zinahitaji ufuatiliaje katika maeneo yote ya Zanzibar usiku na mchana. Hadi Kamati inatayarisha Ripoti hii katibu mtendaji wa baraza hili bado anatomia usafiri wa Vespa katika shughuli zake zote za kikazi.

1:4:2 Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale

Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale ni moja kati ya Idara zilizomo chini ya Wizara hii na imeundwa kwa mujibu wa Sheria (Sheria ya Mambo ya Kale, nambari 11 ya mwaka 2002) katika kuhakikisha kwamba historia ya Zanzibar na urithi wa utamaduni unahifadhiwa, unaendelezwa na kudumishwa kwa ajili ya maendeleo ya taifa hili.

Kamati iliweza kutembelea baadhi ya Makumbusho ikiwemo Makumbusho ya Taifa – Forodhani, Makumbusho ya Pete, Unguja Ukuu - Kae Pwani, Bikhole Ruins – Bungi, Makumbusho ya Chake Chake - Pemba na Makumbusho ya Urithi wa Tanga.

Mambo ambayo Kamati haikuridhika nayo na Changamoto zinazoikabili Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale

- ✓ **Ujenzi wa Jengo la Beit el Jaibu:** Kusua sua kwa Ujenzi wa Beit el Jaib ambayo ni 'roho' ya historia ya Mji Mkongwe ambapo lawama nyingi huelekezwa kwa watendaji wa Idara hii.
- ✓ **Elimu :** Uelewa mdogo kwa wananchi katika kulinda na kuhifadhi maeneo ya kihistoria nchini.
- ✓ **Uvamizi wa Maeneo ya Kihistoria:** Baadhi ya maeneo ya kihistoria yamekuwa yakivamiwa na wananchi kwa njia mbalimbali kama vitega uchumi, mahoteli, mashamba na makaazi ya watu.
- ✓ **Uchafu:** Majengo mengi ya kihistoria na magofu hayako katika hali nzuri ya usafi licha ya Idara hiyo kuwa na wahudumu wa kutosha.
- ✓ **Matumizi yasiyoridhisha.** Kamati haikuridhika kabisa na matumizi ya Idara hiyo hasa katika ukarabati wa nyumba ya Kihistoria unguja Ukuu na ujenzi wa vibanda Pete Mkoa wa Kusini Unguja.

MAAGIZO YA KAMATI

- (a) Kamati inasisitiza juu ya kuongeza juhudi ya kuyalinda na kuyahami Majengo yote ya Kihistoria ikiwezekana hata kwa ubia, ili kulinda urithi wa historia yetu pamoja na kuongeza mapato ya Idara hii na taifa kwa ujumla.
- (b) Idara iyaoorodheshe na kuyatambua maeneo yote yaliyopimwa, maeneo ambayo hayajapimwa na maeneo wanafikiria kuyatambua na kuyatangaza kuwa ya kihistoria.
- (c) Idara ijenge vyoo vyenye hadhi ya kitalii katika majumba ya kumbukumbu, ili kuondosha tatizo la hivi sasa kwa huduma hiyo hasa kwa wageni.

1:5 SEKTA YA MICHEZO

Sekta ya Michezo ni miongoni mwa sekta zilizoko chini ya Wizara ya Habari, Utalii , Utamaduni na Michezo. Sekta hii inaundwa na Kamisheni ya Utamaduni na Michezo pamoja na Baraza la Taifa la Michezo (BMTZ), ambazo kiujumla zinajukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Michezo Zanzibar pamoja na kuhakikisha kuwa vyama vya michezo vinafanya shughuli zao za kuendeleza Michezo kwa mujibu wa katiba na sheria zinazoongoza michezo husika.

1:5:1 Uendelezaji wa Miundombinu ya Michezo

Kamati imebaini kwamba kwa mara ya kwanza katika Historia ya Michezo Zanzibar, Wizara kupitia Sekta hii imeweza kusimamia upimaji wa maeneo maalum ya michezo mijini na vijijini. Matayarisho ya Ujenzi katika Uwanja wa Tumbaku, Maisara, na Nungwi pamoja na Matengenezo ya Uwanja wa Mao Tse Tung yanatoa ishara njema ya kuimarisha michezo hapa Zanzibar.

1:5:2 Ushiriki wa Zanzibar katika michezo ya Kimataifa.

Katika nyakati tofauti katika mizunguko ya kazi za Kamati, kamati imeonana na Viongozi wenye dhamana ya michezo na kueleza Kamati kwamba timu za Zanzibar zimekua zikishiriki katika mashindano mbalimbali ya kimataifa yanayoandaliwa kila mwaka na mashirikisho ya Kimataifa na kuitangaza nchi yetu Kimichezo.

Kamati inatambua Mchango wa Wizara na Serikali kwa ujumla kupitia Idara yake ya Michezo. Kamati imebaini kwamba Idara ya Michezo imezisaidia timu za Taifa za

Mchezo wa Judo iliyoshiriki mashindano ya Afrika Mashariki na Kati, mchezo wa Riadha, Wanyanyua Vitu Vizito, Timu ya mpira wa miguu ya Zanzibar Heroes, Netiboli , timu ya michezo ya Viziwi, Chama cha Michezo ya Watu wenye Ulemavu wa akili na kupata Medali za dhahabu, fedha na shaba.

1:5:3 Zanzibar Heroes na Zanzibar Sand Heroes

Katika kipindi hiki cha mwaka 2017/2018 Zanzibar imeweza kujitangaza Uimwenguni kupitia timu ya Taifa ya michezo Zanzibar (**Zanzibar Heroes**) baada ya kufanikiwa kupata nafasi ya Makamo Bingwa katika mashindano ya **Senior Challenge Cup,2017** yaliyofanyika nchini Kenya ambayo yaliandaliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Aidha Timu ya Mpira wa ufukweni (**Zanzibar Sand Heroes**) nayo imefanikiwa kupata ushindi wa kwanza katika mashindano ya **Copa Beach Soccer** yaliyofanyika Dar es Salaam. Kamati inatoa pongezi za Dhati kwa timu zetu hizi kutokana na mafanikio na ushindi huo mkubwa ambao umeiletea sifa kubwa nchi yetu.

Mambo ambayo Kamati haikuridhika nayo na Changamoto katika Sekta ya Michezo

- ✓ **Ufinyu wa Bajeti:** Wizara na Serikali kwa ujumla inafahamu kwamba, timu zetu zinashiriki mashindano ya kimataifa kila mwaka wakati hivi sasa hali ya fedha za michezo zinazotengwa ni kidogo na hazikidhi mahitaji ya vilabu mbali mbali vinavyoshiriki michezo ndani na nje ya nchi.
- ✓
- ✓ **Kuomba kwa Wafanyabiashara:** Kutokana na bajeti ndogo inayotengewa Baraza la Michezo, watendaji wa Baraza hilo wanabakia kuwa ombaomba hasa kwa wafanyabiashara hadi kufikia hatua ya Mfanyabiashara mmoja kuisaidia BTMZ wakati wa Mashindano ya **Senior Challenge Cup,2017** na baadae kulazimisha atangazwe ndani ya Baraza la Wawakilishi kitu ambacho ni kinyume na utaratibu.
- ✓ **Ruhusa za Wachezaji :** Baadhi ya timu zenye wachezaji kutoka Zanzibar ambao wameitwa kambini kwa Timu ya taifa ya Zanzibar kunyimwa ruhusa na timu zao.
- ✓ **Mfumo wa Kuibua vipaji:** Kutokua na mfumo unaotambulika wa kuibua na kuvuna vipaji vya wanamichezo.

MAAGIZO YA KAMATI.

1. Wizara iongeze Bajeti katika sekta ya Michezo ili kuimarisha vilabu na wanamichezo wetu hasa wale wanaoshiriki katika mashindano ya Kimataifa na kujiepusha na mtindo wa kuwa ombaomba.
2. Wizara ya Habari, Utalii , Utamaduni na Michezo ikae pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iangalie uwezekano wa Kurejesha ari na Mvuto wa Mashindano ya Michezo ya elimu bila ya malipo ikiwa ni njia moja wapo ya kuibua vipaji vya wanamichezo wetu.
3. Wizara iangalie upya viwango Viingilio vya Mchezo wa mpira wa miguu ili kuwawezesha wapenzi wa mchezo huo waweze kuvimudu kwa lengo la kuwaongezea ari na ushabiki wa mpira hapa Zanzibar.

2. WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO

2:0 Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee , Vijana, Wanawake na Watoto

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee , Vijana, Wanawake na Watoto ni miongoni mwa Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo inajukumu yafuatayo;-

- a) Kusimamia Mpango Mkuu wa Ajira kwa Vijana na utekelezaji wa Sheria za kazi.
- b) Kupanua program za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na Kuimarisha Mfumo wa Ushirika.
- c) Wizara inajukumu la Kuimarisha Mfumo wa Uratibu,ufuatiliaji na Tathmini kwa program za Hifadhi ya Jamii na Vijana, Wazee, Wanawake na Watoto.
- d) Kukuza Usawa wa Kijinsia na Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wa wanawake na Watoto.

Wizara inatekeleza malengo hayo kwa Kupitia taasisi zifuatazo;-:

1. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
2. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
3. Idara ya Ajira;
4. Idara ya Usalama na Afya Kazini;
5. Idara ya Maendeleo ya Ushirika;
6. Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii;
7. Idara ya Maendeleo ya Vijana;
8. Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto;
9. Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
10. Kamisheni ya Kazi; na
11. Ofisi Kuu, Pemba.
12. Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ; na
13. Baraza la Vijana.

BAJETI YA WIZARA:

Kwa mwaka wa fedha **2017/2018**, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, iliidhinishiwa jumla ya shilingi **14,456,640,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Programu na majukumu ya Wizara. Pia Wizara Ilikadiriwa kukusanya Tsh

891,078,000 na hadi kufikia Disemba 2017 ilikusanya Tsh.399,712,750 sawa na asilimia 45.

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari, na Utalii imeridhika ha hatua za Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Wizara huko Mwanakwerekwe ambalo linakusudiwa kuwa la Ghorofa mbili. Kamati imeshuhudia kukamilika kwa Ghorofa ya Kwanza na imearifiwa kwamba hivi sasa Wizara imo katika maandalizi ya kuendelea na ujenzi huo katika ghorofa ya Pili.

Katika mwaka huu wa fedha, Wizara inaendelea kutekeleza program zake tano (5) zifuatazo:

1. Program ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi
2. Programu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji Wanawake
3. Programu ya Kuimarisha Huduma za Ustawi
4. Programu ya Uongozi na Mipango ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
5. Programu ya Kuratibu uzalishaji, Upatikanaji wa Ajira za Staha na Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria.

2:1 SEKTA YA KAZI:

Sekta hii ni miongoni mwa sekta muhimu inayosimamiwa na Wizara hii, katika utekelezaji wa kimajukumu ya sekta hii, Idara ya Ajira, Kamisheni ya Kazi pamoja na Idara ya Usalama na Afya Kazini, zinahusika moja kwa moja na sekta hii.

2:1:1 Kamisheni ya Kazi

Kamisheni ya kazi imeundwa rasmi kwa mujibu wa sheria ya Ajira Nam.11 ya mwaka 2005 na ina Idara Mbili ambazo ni Idara ya Ajira pamoja na Idara ya Usalama na Afya Kazini. Kamati inafahamu kwa majukumu makubwa ya Kamisheni ni Kusimamia Utekelezaji wa Sheria za Kazi, Kufanya Ukaguzi Kazi, Kusuluhisha Migogoro ya Kazi pamoja na kukuza Mahusiano mema Kazini.

Kwa Mujibu wa Taarifa za Kamisheni hii, hadi mwishoni mwa mwezi Disemba 2017, jumla ya taasisi 260 za Unguja na Pemba zilikaguliwa ili kufuatilia ulipaji wa kima kipya cha chini cha Mshahara kwa sekta binafsi.

Aidha Kwa kipindi cha Julai- Disemba takwimu zinaonesha kwamba kuna jumla ya raia wa Kigeni 942 ambao wamepatiwa Vibali vya Kazi na Kuingizia mapato ya Tsh.329.301,000= kwa Kamisheni.

2:1:2 Idara ya Ajira.

Idara ya Ajira ni Miongoni mwa taasisi iliyopo katika Kamisheni ya Kazi ambapo majukumu makubwa ya Idara hii ni Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ajira pamoja na kubuni, kusimamia mipango na taratibu za soko la Ajira.

Ajira Nje ya Nchi

Kamati imebaini kwamba hadi kufikia tarehe 30 Disemba 2017, Idara kwa kushirikiana na Wakala Binafsi wa Ajira na Balozzi za Tanzania zilioko nchi wanakokwenda imefanikiwa kuwapatia ajira Vijana **620** (171 wanaume na 449 wanawake) waliokwenda katika nchi za Bahrein, Maldieves, Oman, Qatar, Saud Arabia na Umoja wa Falme za Kiarabu. Aidha kamati imebaini kwamba Idara imeweza kuwafanyia Ukaguzi na kuwapa miongozo Mawakala 10 wa ajira za Nnje ya nchi.

2:1:3 Idara ya Usalama na Afya Kazini

Idara ya Usalama na Afya Kazini imeundwa mwaka 2011 chini ya Kifungu nambari 4 cha Sheria ya Usalama na Afya kazini, Sheria nambari 8, ya mwaka 2005 ikiwa na jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria hiyo. Majukumu mengine ya Idara hii ni kuandaa miongozo ya Utekelezaji wa masuala ya afya na usalama kazini pamoja na kuzifanyia ukaguzi sehemu za kazi. Hadi kamati inatayarisha taarifa hii, ajali 8 zimeripotiwa na kuchunguzwa na idara hii ikiwa zaidi ni Mahotelini na Vituo vya mafuta.

Ziara za Kamati Sehemu za Kazi

Wakati wa kazi za Kamati, Kamati yetu ilizitembelea sehemu mbali mbali za kazi kuangalia utekelezaji wa majukumu na sheria zinazohusiana na sekta hii . Miongoni mwa taasisi tulizotembelea ni kama ni Zanzibar Serena Hotel, Kampuni ya Ujenzi (Coast Construction) – Kiponda, Zanzibar Petroleum LTD, Zanzibar Milling Corporation, Kiwanda cha maji "Drop of Zanzibar " - Jendele, Kampuni ya Uchunguzi wa mafuta kwa njia ya Miripuko na Mitetemo "BGP" Marumbi, The Aiyana Hoteli- Makangale, Manta Resort – Makangale, Fundu Lagon – Mkoani, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Migogoro ya Kazi)- Tanga , Bandari ya Tanga Kiwanda cha Tanga Fresh Milk na Kiwanda cha Tanga Cement.

Mambo ambayo Kamati haikuridhika nayo na Changamoto katika Sekta ya Kazi

- ✓ **Ufuatiliaji Mdogo:** Maafisa wa Ukaguzi kazi na Usalama wa Afya Kazini hawafuatilia majukumu yao hasa katika Sekta Binafsi hatua ambayo imeifanya Kamati hii kufika katika Kampuni ya Ujenzi (Coast Construction) – Kiponda mara mbili na kutoa maagizo kadhaa ya kufuatiliwa ikiwemo mikataba ya kazi na utekelezaji wa agizo la kima cha chini, lakini maafisa hao hawakutekeleza hata moja.
- ✓ **Ubadhirifu wa Baadhi ya watendaji wa Ukaguzi Kazi:** Kamati imebaini kwamba baadhi ya maafisa wa Ukaguzi Kazi na Usalama wa Afya Kazini wamekuwa wakitumiwa kwa ubadhirifu kwa kuwashawishi waajiri kutotekeleza Sheria za kazi ikiwemo malipo ya Kima cha chini kwa kuwakandamiza wazalendo na kuwapendelea wageni.
- ✓ **Wazalendo Kukosa Ajira:** Ajira Binafsi kuwa na wageni wengi kulikowazalendo.
- ✓ **Mishahara:** Taasisi binafsi kutolipa mishahara kama serikali ilivyooagiza.
- ✓ **Michango ya ZSSF :** Taasisi binafsi kutochangia michango ya ZSSF kama inavyotakiwa.

MAAGIZO YA KAMATI:

1. Kamati inaitaka Wizara kupitia Kamisheni ya Kazi kufuatilia kwa ukaribu zaidi suala la madai ya haki za wafanyakazi wa Kampuni ya Ujenzi (Coast Construction) ya Kiponda pamoja na Kampuni ya Uchunguzi wa mafuta kwa njia ya Miripuko na Mitetemo BGP –Marumbi.
2. Wizara ihakikishe kwamba wafanyakazi wa Manta Resort – Makangale Na Kampuni ya Ujenzi (Coast Construction) na BGP Makato ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ZSSF yanafikishwa kunakohusika.

3. Kamati inaitaka Idara ya Ajira kuandaa mkakati maalum wa kutoa taaluma kwa wafanyakazi wa umma yaani, serikali pamoja na taasisi ama kampuni binafsi kuomba taarifa za michango yao Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) kwa waajiri wao , kwa lengo la kuepusha usumbufu hapo baadae.
4. Maafisa wa Kamisheni ya Kazi wafanye ukaguzi kazi mara kwa mara hasa katika sekta binafsi, ili kuepusha migogoro inayojichomoza mara kwa mara kuhusiana na haki za wafanyakazi.
5. Kamisheni iwachunguze vizuri baadhi ya Maafisa wake kutokana na tuhuma za kuwa wasaliti na kuwashawishi baadhi ya waajiri wasitekeleze sheria za kazi pamoja na Maagizo yanayotolewa na Serikali.
6. Kuweko na Sera yenye kutilia mkazo ajira kwa wazalendo.

2:2 SEKTA YA UWEZESHAJI.

Sekta hii ina umuhimu wa kipekee katika kuhakikisha kwamba Wananchi wanawezeshwa katika kujikwamua na hali ya umaskini. Uwezeshaji unaofanyika ni kwa kupitia njia mbali mbali ambazo Serikali kupitia Wizara hii imezianzisha kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo. Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Idara ya Maendeleo ya Ushirika; na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ndizo zinazohusika kwa ukaribu zaidi katika kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa kwa ufanisi.

a) Mfuko wa Uwezeshaji

Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ulizinduliwa rasmi Disemba 2013, ukiwa na lengo la kuwapatia wananchi huduma za kifedha ili waweze kufanya shughuli za uzalishaji kwa lengo la kunyanyua hali zao za maisha. Aidha Kamati imebaini kwamba Mfuko unalenga zaidi kutoa mikopo yenye masharti nafuu, ili kuongeza fursa za ajira hasa kwa Vijana, Wanawake na makundi Maalum.

Mfuko huu pia umerithi wateja waliokuwa wa mfuko wa kujitegemea pamoja na wateja wa ulikua Mfuko wa AK/JK.

b) Utoaji na Urejeshwaji wa Mikopo

Kamati imegundua kwamba katika kipindi cha Miaka minne (**Hadi kufikia Disemba 31 , 2017**) Mikopo 1,430 yenye jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tano Sabiini na Mbili, Elfu na Elfu Sabiini na Tano (**2,572,075,000/=**) imetolewa Unguja na Pemba ambapo wananchi 21,629 wamefaidika moja kwa moja na mikopo hiyo (wanawake 12,031 na wanaume ni 9,598).

Kwa mujibu wa ripoti za Mfuko wa Uwezeshaji tokea kuanza kutolewa kwa Mikopo hiyo Mwezi Juni 2014, Jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nane na Tisini na Sita, Mia Tano na Tano (1,496,666,505/=) sawa na asilimia 96 ya marejesho waliyotarajiwa kukusanya.

c) Vyama vya Ushirika:

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake , Habari na Utalii inapongeza uwamuzi wa serikali wa kuanzisha Idara ya Maendeleo ya Ushirika, Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Mfuko wa Uwezeshaji lengo ikiwa ni kuratibu , kutoa mikopo pamoja na misaada kwa wajaasiriamali na wananchi kwa ujumla ikiwa ni mtu mmoja mmoja ua waliojikusanya kwa pamoja kwa kuunda vikundi vya ushirika na hatimae kuwaondelea umasikini. Hata hivyo, Kamati haijaridhika na utekelezaji wa azma hiyo.

Kamati imepata fursa ya wananchi mbali mbali waliowezeshwa pamoja na vyama mbali mbali vya ushirika Pemba , Unguja na Tanga ili kuona ni jinsi gani wananchi wanajikita katika kufanya shughuli mbali mbali za kujiletea maendeleo baada ya uwezeshwaji huo. Katika ziara hizo, Kamati imebaini kwamba bado wananchi wanahamasika na wanamwamko wa Kujiendeleza na baadhi yao wamefanikiwa katika vikundi vyao. Kamati inachukua fursa hii kukipongeza kwa dhati kabisa Kikundi cha ushirika wa Kilimo cha ndimu cha **Juhudi zetu Bwejuu- Dongwe** , kikundi ambacho kinapaswa kupigiwa mfano kwa mafanikio makubwa waliyopata baada ya kuwezeshwa na Wizara, na kutumia vizuri mikopo wanayopatiwa na hatime kuweza kubadilika katika hali zao za maisha kwa kuongeza vipato vyao na ajira. Kamati ilibaini kwamba Kikundi kilikopeshwa Jumala ya **Shilingi 39,000,000/=** kwa awamu mbili na hivi sasa tayari kimerejesha **asilimia 66** ya mkopo huo.

Mmoja wa Wakulima hao amesema hivi sasa kazi zake za kilimo cha ndimu zinaendelea vizuri na amekua akivuna mapoloo kadhaa kwa siku kiasi ambacho ameweza kuwaajiri akinamama 15 ambao huwalipa ujira wao kila siku na pia huwarejesha nyumbani kwa usafiri wa gari ambayo anajivunia kwamba amepata kutokana na faida ya kilimo chake cha ndimu.

Mambo ambayo Kamati haikuridhika nayo na Changamoto katika Sekta ya Uwezeshaji

- 1. Takwimu sahihi :** Hakuna takwimu sahihi za idadi ya vyama au mtu mmoja mmoja walioweza na Mifuko ya Uwezeshaji (Mfuko wa Kujitegemea, Mfuko wa AK/JK na Mfuko wa Uwezeshaji) ambao wameweza kufanikiwa kutoka hali ngumu ya Umasikini na kuweza kujitegemea (*From Zero to Hero.*)
- 2. Ukosefu wa Soko:** Wajaasiriamali wamekuwa wakijitahidi sana kuzalisha hasa kilimo cha matunda lakini wamekuwa wakivunjika moyo kutokana na tatizo sugu la ukosefu wa soko la bidhaa zao. Baadhi ya Vikundi vya Ushiriki vilivyotembelewa na Kamati na kugundua tatizo la ukosefu wa Soko ni Matuleni (furniture),GAPE SACCOS –Kizimbani Wete (Usarifu wa Mazao na Ufumaji), Bau Business Group _ Karakana Unguja (Kukoboa Mazao/uchongaji) na Num Tailoring Jumbi (ushoni).
- 3. Ukosefu wa Mfumo wa Usindikaji wa Bidhaa:** Hakuna mfumo na Viwango bora vya usindikaji na usarifu wa bidhaa zinazozalishwa na vikundi vyetu.
- 4. Bei kubwa ya Pembejeo :** Bei kubwa ya pembejeo za Kilimo , hasa kilimo cha Maweni pamoja na taaluma ndogo kuhusiana na shughuli zao bado zinakwaza katika kutekeleza vyema majukumu yao.
- 5. Urejeshaji wa Mikopo:** Baadhi ya wakopaji kutotaka kulipa mikopo yao bila ya sababu za msingi jambo ambalo hupelekea kuwanyima fursa wananchi wengine kupata huduma hii.

MAAGIZO YA KAMATI:

1. Kamati inaiagiza Wizara ishirikiane na Wizara ya Biashara na Viwanda ili kuangalia uwezekano wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya usarifu wa mazao au kutafuta wawekezaji ama kuingia ubia ili kuyahami mazao ya wakulima wetu.
2. Kamati inaishauri wizara na serikali kwa ujumla kuangalia uwezekano wa Kupunguza bei za Pembejeo kwa wakulima wa maweni ambao hivi sasa wako mstari wa mbele katika kilimo cha Ndimu, machungwa na tungule kilimo ambacho hivi sasa kinakubali vizuri katika maeneo mbali mbali.
3. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha iangalie uwezekano wa kuanzisha Benki ya Ushirika hapa Zanziabar.

2:3 SEKTA YA WAZEE.

Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii ambayo ipo chini ya Wizara hii inahusika kwa ukaribu zaidi. Idara hii inajukumu la kusimamia Ustawi wa Wazee, Uimarishaji wa Hifadhi ya Jamii na Watoto, Ulipaji Fidia na Ustawi wa Jamii kwa Ujumla. Kamati katika kufuatilia kwa kiasi gani Wizara inawashughulikia wazee, ilipata fursa ya kuzitembelea nyumba za wazee zilizopo Unguja (Sebleni na Welezo na Pemba (Limbani) na kupata fursa ya kuzungumza na wazee waliopo katika nyumba hizo, ambako kwa kweli kamati imeridhika kabisa na namna wazee wanavyotunzwa katika nyumba hizo.

Wazee hao walipongeza utaratibu mzuri wa Mlo pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein kwa imani yake juu ya wazee wote nchini.

2:4 SEKTA YA VIJANA:

Wizara hii pia imepewa jukumu la kuhakikisha kwamba Vijana ambao ndio kundi lenye idadi kubwa ya watu katika nchi yetu, linasimamiwa ipasavyo katika kuhakikisha linafikia malengo yao. Katika usimamizi wa sekta hii, serikali ilianzisha Idara ya Maendeleo ya Vijana na Baraza la Vijana vyote kwa pamoja kwa ajili ya Kusimamia na Kuratibu kwa ukamilifu shughuli zote za Vijana pamoja na kuhakikisha kwamba sheria zote zinazokusudiwa kurahisisha maendeleo ya Vijana zinatekelezwa ipasavyo. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuhakikisha kwamba malengo ya Sekta hii yanafikiwa hasa kwa kufanikisha kuzinduliwa rasmi kwa Baraza la Vijana hivi karibuni. Kamati inaomba changamoto ndogondogo zilizo katika sekta hii ziendelee kutatuliwa ili Vijana waweze kufikia malengo yao kama ilivyokusudiwa.

2:5 SEKTA YA WANAWAKE NA WATOTO

Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto inajukumu la Kuratibu na kusimamia Shughuli za kuwaendeleza wanawake na watoto pamoja na program ya kukuza muitikio wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mambo ambayo Kamati haikuridhika na Changamoto katika Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto.

- ✓ **Ukosefu wa Usafiri:** Kamati haikuridhika na tatizo la ukosefu wa usafiri katika Idara hii hasa kutokana na majukumu ya utendaji wa idara ikiwemo ufuatiliaji wa masuala ya Kesi za udhalilishaji.
- ✓ **Kukosekana Mfumo bora wa Ufuatiliaji wa Kesi za Udhalilishaji:** Idara haina mfumo bora na unaoeleweka wa ufuatiliaji wa kesi za udhalilishaji kuanzia shehia hadi taifa.
- ✓ **Waratibu wa Shehia kukosa vitambulisho:** Kukosekana kwa vitambulisho vya Waratibu wa Wanawake na Watoto wa Shehia kunachangia kukosekana kwa ushirikiano mzuri baina ya Waratibu na wasimamizi wa sekta za kisheria pamoja na Waratibu kukosa moyo wa kufanyakazi kutokana na kutolipwa posho.

UDHALILISHAJI WA WANAWAKE NA WATOTO.

Kamati inaendelea kusioneshwa na kusikitishwa juu ya kushamiri vitendo vya ukatili , udhalilishaji wa wanawake na watoto , mapenzi ya Jinsia moja na matumizi ya Dawa za kulevya katika jamii yetu. Kamati inaamini kwamba vitendo hivi vimeshamiri katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu, hivyo sote kwa pamoja tuunganishe nguvu zetu kuvipiga vita na hatimae kuvitokomeza kabisa.

Kamati hairidhiki kabisa na baadi ya watendaji wanaohusika na kushughulikia vitendo vya udhalilishaji wakiwemo Maafisa wa Idara ya Wanawake na Watoto, watendaji wa Jeshi la Polisi, Madaktari na watendaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahkama wanaoshughulikia kadh-ya hii.

Pamoja na juhudi za Kitaifa za kupambana na vitendo vya udhalilishaji, vitendo hivyo bado vimekua vikiongezeka Unguja na Pemba . Kwa kuona Uzito wa jambo hili kamati iliweka Utaratibu Maalum wa kufuatilia mwenendo wa vitendo hivi katika jamii, Idara ya Maendeleo ya Wanawake pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika mizunguko yake yote mwaka huu.

2:5:1 Maendeleo ya Kesi za Udhalilishaji - Unguja

Kulingana na Takwimu za Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa awamu ya Kwanza (Kipindi cha Machi-Disemba,2017) ilifungua jumla ya Kesi 55 katika Ngazi ya Mahkama Za Mkoa, Wilaya na Watoto. Kati ya kesi hizo 55 tayari kesi 43 zimemalizika ambapo kesi 20 washtakiwa wamekutwa na hatia, kesi 20 washtakiwa wameachiwa huru na kesi 3 zimeondoshwa (zimeondoshwa na upande wa Mashtaka chini ya kifungu cha 100(a)). Kesi 12 bado zinaendelea katika hatua mbali mbali ambapo kesi 8 ziko katika hatua za usikilizaji wa mashahidi, na kesi 8 zipo katika hatua za utetezi.

Maelezo zaidi ya kesi hizi yanaonekana katika Jedwali zifuatazo;-

a) Mahkama za Mkoa

Mahkama	Vuga	Mfenesini	Mwera	Jumla
Idadi ya Kesi	27	8	4	39
Usikilizaji Mashahidi	7	0	0	7
Utetezi	1	0	0	1
Zilizoondolewa -Chini ya Kif. 100(a)	2	0	0	2
Zinazosikilizwa	1	1	0	2
Zenye Hatia	10	3	1	14
Zisizokua na Hatia	6	4	3	13

Chanzo, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

b) Mahkama za Wilaya

Mahkama	Mwanakwerekwe	Makunduchi	Jumla
Idadi ya Kesi	8	2	10
Usikilizaji Mashahidi	0	1	1
Utetezi	0	0	0
Zilizoondolewa - By Court(Under 209)	1	0	1
Zinazosikilizwa	0	0	0
Zenye Hatia	3	0	3
Zisizokua na Hatia	4	1	5

Chanzo, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

c) Mahkama za Watoto.

Mahkama	Mahonda	Vuga	Jumla
Idadi ya Kesi	2	4	6
Usikilizaji Mashahidi	0	0	0
Utetezi	0	3	3
Zilizoondolewa	0	0	0
Zinazosikilizwa	0	0	0
Zenye Hatia	2	1	3
Zisizokua na Hatia	0	0	0

Chanzo, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

2:5:2 Maendeleo ya Kesi za Udhalilishaji – Pemba

Kamati pia wakati ilipokua katika kazi zake huko Pemba ilifika katika Ofisi za Mkurugenzi wa Mashtaka Ofisi ya Pemba ambako iliaarifiwa kwamba Jumla ya majalada 78 ya kesi za udhalilishaji yalipokelewa kwa kipindi cha Julai- Disemba 2017. Majalada hayo yanonesha kwamba Kutoka Wilaya ya Mkoani yalipokelewa majalada 10 ambapo majalada 9 yaliidhinishwa kufunguliwa kesi na jalada moja Afisi hiyo ilielekeza lifanyiwe marekebisho. Kutoka Wilaya ya Chake Chake majalada yaliyopokelewa ni 34 ambapo majalada 29 yaliamuliwa kwenda Mahkamani na majalada 5 yafanyiwe marekebisho.

Kamati pia imebaini kwamba kutoka Wilaya ya Wete yalipokelewa majalada 22 ambapo majalada 18 yaliamuliwa yaende Mahkamani na majalada 3 yafanyiwe marekebisho na jalada 1 lilifungwa. Kutoka Wilaya ya Micheweni majalada 12 yalipokelewa ambapo 11 yaliamuliwa yaende Mahkamani na 1 lifanyiwe marekebisho.

Kwa ujumla, kwa Mikoa yote miwili ya Pemba kati ya majalada 78 yaliyopelekwa majalada 67 yaliamuliwa na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka yapelekwa Mahkamani, majalada 10 yafanyiwe marekebisho na 1 lilifungwa.

Hata hivyo, taarifa kutoka ndani ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka majalada yaliyopelekwa Mahkamani katika kipindi hicho ni 36 ambapo kutoka Wilaya ya Mkoani ni 5, Wilaya ya Chake Chake 19 na 9 katika Wilaya ya Wete wakati Wilaya ya Micheweni ni 3. Hii inaonesha kwamba majalada 31 bado yalikuha hayajapelekwa Mahkamani katika kipindi hicho licha uamuzi wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwamba yapelekwe Mahkamani.

Kamati imearifiwa kwamba Kesi zote 36 zilizofunguliwa Mahkamani zinaendelea katika hatua mbali mbali mbali ambapo baadhi zinasikilizwa ushahidi wa upande wa Mashtaka, nyengine zipo katika hatua za uamuzi mdogo na baadhi zinasubiri hukumu.

2:5:3 Matayarisho ya Awamu ya Tatu ya Operesheni ya Kesi za Udhalilishaji.

Kamati inapongeza sana juhudi zinazochukuliwa na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kufanya mikakati ya makusudi ya kuzishughulikia Kesi za Udhalilishaji kwa opereshini Maalum. Kamati imearifiwa kwamba imo katika matayarisho ya ufunguaji wa kesi za udhalilishaji awamu ya tatu. Zowezi hili linategemewa kuanza mwezi wa Februari 2018, ambapo jumla ya majalada **290** yanashughulikiwa na wanasheria wa Afisi hiyo kwa hatua za mwisho.

Changamoto katika Kesi za Udhalilishaji

Baada ya Kamati kutembelea Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na sehemu kadhaa kufuatilia kesi hizo, Kamati imebaini kwamba kumekua na changamoto Kadhaa zinazokwamisha kesi za udhalilishaji hapa Zanzibar. Baadhi ya Changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

- a) Uwepo wa maombi mengi ya ufutishaji wa kesi za udhalilishaji kutoka kwa wanajamii, hii inatokana na baadhi ya wahanga kuowana na washtakiwa au uhusiano wa karibu wa familia.**
- b) Baadhi ya Watendewa wa makosa ya udhalilishaji umri wao ni mdogo sana na wanashindwa kujieleza Polisi au kutoa ushahidi mahkamani.**
- c) Kuwepo kwa kasoro katika baadhi ya Hati za Uchunguzi wa kidaktari (PF3) kwa watendewa na kupelekea kukosekana kwa ushahidi.**
- d) Kucherewa kuripotiwa kwa matukio ya Udhalilishaji kutokana na sababu mbali mbali kama vile umbali wa vituo vya Polisi, elimu ndogo ya wanajamii kuhusu vitendo husika.**
- e) Kukosekana kwa umahiri wa kutoa ushahidi kwa baadhi ya mashahidi (Vigeu geu na Wakaidi) ambapo wengine inawezekana ukweli wanaujua lakini wanakuwa na woga Mahkamani na wengine huwa ni wakaidi au kukataa kuzungumza Mahkamani.**

f) Baadhi ya watendaji wa makosa hayo kuonekana wakidunda mitaani siku chache baada ya kufanya makosa hayo.

g) Kukosekana kwa Maadili kwa baadhi wa Watendaji wanaosimamia haki jinai.

h) Kauli za baadhi ya Watendaji wanaosimamia haki jinai (Mfano Majibu ya Mkuu wa Kituo cha Polisi Nungwi kwa kamati kuhusiana na watuhumiwa wa Udhalilishaji yaliyoripotiwa Kituoni hapo).

Maoni na Ushauri wa Kamati

1. Taasisi za kudhibiti Jamii (social Control) zitimize wajibu wake ;-
 - Familia – Malezi na maadili mema
 - Taasisi za Kijamii (Shule na Madrasa) – zitayarishe raia wema
 - Dini – zitolie Mkazo kukataza maovu
 - Sheria – zidhibiti watenda makosa
 - Haki jinai (Criminal Justice) – watendaji wawe weledi na waadilifu
2. Kamati inashauri kuangaliwa upya na hatimae kuikata kabisa misingi ya udhalilishaji na vitendo viovu ikiwemo; Kuongezeka kwa kasi kubwa kwa kumbi za starehe katika maeneo yetu, Baa za mitaani, Mitandao ya kijamii isiyodhibitiwa, Kumong’onyoka kwa maadili, Visingizio vya sherehe mbalimbali zisizodhibitiwa kama vile “Day OUT” , “Birthday” , Singo , ‘Kibuki’ nk.
3. Kutolewa elimu ya mara kwa mara kwa wanajamii kuhusiana na vitendo vya udhalilishaji na sheria zinazohusiana na vitendo hivyo.
4. Serikali ihakikishe kwamba inaweka watendaji wenye uweledi na wanaofuata Maadili ya kazi zao katika sehemu zote za huduma.

5. Kufanya vikao vya mara kwa mara na wapelelezi wa kesi za udhalilishaji.
6. Kuandaliwa kwa mafunzo maalum kwa madaktari kuhusu namna ya Kufanya uchunguzi kwa watendewa wa makosa ya udhalilishaji na taarifa zinazostahiki kujazwa vizuri katika PF3
7. Kukataa maombi yote ya wanajamii yanayokusudia kufutisha kesi za udhalilishaji.

2:5:4 Mswada wa Sheria ya Adhabu na Sheria ya Mwenendo wa Jinai

Wakati Kamati ikiwa katika hatua za mwisho za kukamilisha Ripoti yake, Serikali kupitia Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilikua tayari imeandaa rasimu ya **Mswada wa Sheria ya Adhabu na Sheria ya Mwenendo wa Jinai** ambao kwa wakati huo ulikuuwa katika ngazi ya Kamati ya Baraza.

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Habari na Utalii, imefurahishwa na kupongeza kwa dhati Dhamira ya Serikali kuja na Miswada hiyo kwani , Kamati inaamini Kwamba itasaidia kupunguza wimbi la Vitendo vya udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto hasa katika Sehemu ya Kumi na Tatu ya Sheria ya Adhabu ambayo inahusika na **Makosa dhidi ya Maadili** ikiwemo, Kubaka, Adhabu ya kubaka kwa kundi, Kujaribu kubaka, Kutorosha mwanamke, Kutorosha watoto wa kike na kiume, Shambulio la aibu, Kunajisi mtu mwenye ulemavu wa akili, Kuwezesha ukahaba na mengineyo. Aidha Kamati inapongeza na kuunga Mkono **Sehemu ya Kumi na Nne** inayozungumzia makosa yanayohusina na ndoa na mahusiano ya kifamilia ikiwemo Ndoa ya hadaa , Kufunga ndoa kinyume na sheria, Ukatili kwa watoto, Kutelekeza mtoto au mtu mwenye ulemavu.

Kuhusu **Sheria ya Mwenendo wa Jinai**, Kamati inaunga mkono utaratibu wa kiupelelezi na Mahkamama ulioanishwa ikiwa ni pamoja na kuziongezea Uwezo Mahkama za Wilaya na mikoa pamoja na kutowapa dhamana watendaji wa makosa haya.

MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaiagiza Wizara kuwahimiza Maafisa wake kushirikiana ipasavyo na waratibu wa Shehia, ili waweze kufuatilia na kusimamia vyema shughuli za wanawake na watoto na kupata takwimu mbali mbali zinazohusiana na shughuli zao.
2. Wizara ishirikiane na Serikali za Mitaa ili kuangalia uwezekano wa Kupatiwa vitambulisho na kifuta jasho kwa Waratibu wa Shehia.
3. Wizara kwa kushirikiana na kukaa pamoja na Serikali za Mitaa, Jeshi la Polisi, Madaktari, Afisi ya DPP na Mahkama ili kuandaa mkakati wa pamoja wa kushughulikia ipasavyo na kwa ufanisi zaidi kesi zote zinazohusika na udhalilishaji.

2:6 Nyumba ya Watoto Mazizini

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina historia ndefu ya kusimamia haki, ustawi na maendeleo ya mtoto tokea baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964. Rais wa kwanza wa Zanzibar Marehemu Abeid Amani Karume aliamua kukianzisha kituo cha kulelea watoto Forodhani, ili kuwatunza watoto ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwahudumia na kuwapatia mahitaji yao ya lazima , vilevile kuwanusuru watoto wasitupwe.

Wakati wa uongozi wa Awamu ya Sita kulitolewa uwamuzi wa Kuwahamisha watoto katika jengo la Forodhani na kuhamia Mazizini kutokana na kuchakaa kwa jengo la Forodhani, jengo kutokua na mwangaza wa kutosha, usalama mdogo wa watoto kutokana na ukuaji wa shughuli za kitalii hapa Zanzibar.

Hadi kufikia mwezi Disemba 2017, Nyumba ya Mazizini ina jumla ya watoto 38 (wanawake 19 na wanaume 19) ambao wanahudumiwa na wafanyakazi 33 katika seksheni tofauti ambapo kamati baada ya Kutembelea Nyumba hiyo imeridhika kabisa na huduma wanazopatiwa watoto kituoni hapo.

Mambo ambayo Kamati haikuridhika nayo na Changamoto

Katika Nyumba ya Watoto - Mazizini

- ✓ **Uhaba wa wafanyakazi :** Nyumba ya kulelea watoto Mazizini inakabiliwa na tatizo la uhaba wa wafanyakazi katika kitengo cha malezi na busatani, tatizo ambalo linatokana na baadhi ya walezi kustaafu.
- ✓ **Uvamizi na wizi:** Uvamizi wa makundi ya wahalifu na wezi ambao huvamia na kuiba baadhi ya vifaa kituoni hapo.
- ✓ **Ukosefu wa Daktari:** Kituo hakina daktari, kitendo ambacho kinawapa wakati mgumu inapotokea dharuru za masuala ya kiafya.
- ✓ **Kufungwa kwa baadhi ya Vyumba na ofisi:** Kamati ilishuhudia kufungwa kwa baadhi ya Vyumba na ofisi katika jengo hilo na hakuna maelezo yoyote kwanini vyumba hivyo vimefungwa na havitumiki, pia Kamati ilitaka kujua nani mmiliki halali wa nyumba hiyo lakini ilikosa majibu.

MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto iangalie uwezekano wa kuvitumia Vikosi vya ulinzi vya SMZ hasa wakati wa usiku badala ya mtindo wa sasa wa kutumia walinzi wa kawaida ili kujikinga na wezi na wavamizi.
2. Wizara izungumze na Wizara ya Afya ili kuangalia uwezekano wa kupatiwa Daktari kituoni hapo.

MAAGIZO YA JUMLA KWA WKUWVWW

1. Tatizo la Usafiri: Kamati imebaini kwamba watendaji wa Wizara hii wanakabiliwa na Tatizo kubwa la usafiri hivyo inaiagiza Wizara ihakikishe kwamba inawapatia usafiri wa Uhakika watendeji wake ili kuwawezesha kufika kwa jamii na sehemu zote za kazi zao na hatimae kuwawezesha kutekeleza vyema majuku yao.

2. Watendji kuacha tabia ya Kujifungia Maofisini: Kamati pia imebaini changamoto kubwa wakati wa ziara yake sehemu za kazi na vijijini kwamba, Maafisa wengi wa Wizara hiyo hawafuatilia ipasavyo majukumu yao. Hivyo, Kamati inaiagiza Wizara kuwafuatilia kwa karibu maafisa wake hao, ili kuhakikisha kwamba wanatekeleza majukumu yao ipasavyo.

SEHEMU YA TATU -

HITIMISHO

3:0 HITIMISHO

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi inawapongeza kwa dhati Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote kwa Ujumla wa Wizara zote mbili zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni.

Aidha, Kamati inatoa shukurani za kipekee kwa Maafisa Wadhamini wa Wizara hizi pamoja na wasaidizi wao wote kwa mashirikiano mazuri waliyoipatia Kamati wakati wote Kamati ilipokuwa Kisiwani Pemba katika kutekeleza majukumu yake.

Vilevile, Kamati inatambua, kuthamini na Kumshukuru Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) pamoja na watendaji wake wote Unguja na Pemba , Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Mkuu wa Wilaya ya Kati, Pamoja na Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa mchango wao mkubwa wa kufanikisha majukumu ya Kamati hii wakati ikifuatalia kadh-ya ya Udhalilishaji hapa nchini.

Kamati pia inatoa Pongeze za Dhati na Maalum kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga pamoja na Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Tanzania Bara kwa mashirikino yao ya dhati kwa kuwa bega kwa bega na Kamati wakati ilipokua Katika ziara za Kimafunzo Huko Tanga na Dar es Salaam.

Mwisho, na kwa umuhimu mkubwa Kamati inampongeza kwa dhati Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika Mhe. Mgeni Hassan Juma, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndg. Raya Issa Msellem, Mratibu wa Kamati Ndg. Ramadhan Khamis Masoud kwa kuiwezesha vyema Kamati kutekeleza majukumu yake na kuweza kutayarisha ripoti yake kwa mwaka 2017/2018. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata.